

Somo la 1: Utangulizi

- Miwani ya kusomea inatumiwa na watu ambao wana shida ya Uoni. Ina msaada mkubwa zaidi katika kusoma. Inasadia watu ambao wana shida ya Uoni kufanya kazi ambazo ziko karibu na mahali walipo (sehemu inayofikika kwa kunyosha mkono)
- Miwani ya kusomea inafanya kazi kwa kukuza maandishi au kuvifaya vitu vionekane vikubwa (vilivyoongezwa ukubwa). Ukubwa wa maandishi au vitu, hutegemea na uwezo wa lenzi.
- Somo hili linazungumzia miwani ya kusomea iliyoainishwa ambayo ina:
 - Uwezo wa kuongeza ukubwa kati ya +1.00 (uwezo wa chini kabisa) to +3.00 (uwezo wa juu kabisa).
 - Lenzi ya kulia na kushoto zenye uwezo sawa

Somo la 2: Ugawaji wa miwani ya kusomea

Chagua



- Anza kwa kufanya uchunguzi wa Afya ya macho kwa kufuata utaratibu wa uchunguzi wa macho wa TAP (au uchunguzi wa macho mwingine wowote unaofanana na ule wa TAP)
- Iwapo skrini ya kuona inaonesha kuwa miwani ya kusomea inaweza kusaidia, mpime mtu vizuri ili aweze kupata miwani stahiki ya kusomea.
- Ili kuweza kupata uwezo sahihi wa lenzi ambayo mhusika anahitaji, muombe mhusika kusoma maneno yaliyoko kwenye E-Chart, aliyoshika mkononi; kwa kuiweka kwenye wa umbali wa sentimeta 40 kutoka kwenye macho yake
- Kama mtu hawezi kuona herufi zilizoko kwenye mstari wa N8, muombe aanze kwa kujaribu miwani yenye uwezo wa chini (+1.00). Endelea kuongeza uwezo wa miwani ya kusomea (hadi kufikia +3.00) hadi mgonjwa atakapokuwa na uwezo wa kusoma vizuri herufi zilizoko kwenye mstari wa N8
- Muulize mhusika kama ana uwezo wa kuendelea kuona vyema N8; ikiwa Chati ya Kuona itaendelea kusogea karibu naye hadi ndani ya urefu wa sentimeta 20 kutoka macho yake.
- Kama itakuwa ngumu kupata miwani ya kusomea ambayo ni sahihi kwake, muelekeze mhusika kwenda kumuona Mtaalam wa Afya ya Macho ili aweze kufanyiwa uchunguzi zaidi.

Kipimo sahihi



- Miwani ya kusomea inapaswa kuwa ni ya kipimo sahihi kinachoendana na uso wa mhusika.
- Ili kupata kipimo sahihi; chagua miwani (frame) ambayo ni kipimo sahihi cha mhusika.
- Kipimo sahihi ni kile:
 - Upana wa miwani: Miwani isiwe mipana kuliko upana wa uso wa mhusika.
 - Kingo ya pua na sehemu ya miwani inasaidia pua kutokuumizwa na miwani: Miwani inapaswa kukaa vyema kwenye sehemu ya pua ya mhusika.
 - Frame (Miwani) inapaswa kukaa vyema kwenye uso wa mhusika.



Matumizi

- Mhusika anaweza kuvaa miwani ya kusomea pale anapohitaji kuona vizuri kitu kilichoko karibu.

- Pamoja na kuvaa miwani ya kusomea, hamasisha watu kusoma kwenye mwanga sahihi ambao wamelekezwa kutumia pale wanaposoma.
- Wafundishe watu namna ya kutunza miwani yao ya kusomea, namna ya kuisafisha na kuangalia nati mara kwa mara.
- Tunza miwani vizuri kwenye kasha lake ikiwa imekunjwa



Ufuatiliaji

- Iwapo mhusika aliyekuja kwa ajili ya kujua maendeleo yake, atakuwa haoni vizuri kama ilivyokuwa hapo awali, fanya uchunguzi wa macho kwa kutumia utaratibu wa uchunguzi macho wa TAP; ili kujua afya ya Macho ya mhusika ilivyo kwa hivi sasa. Chunguza, uwezo wa kuona mbali na karibu. Iwapo uchunguzi huu utaonyesha kuwa miwani ya kusomea bado inafaa; tafuta miwani sahihi zaidi inayoendana na mahitaji ya mhusika.
- Wakati wa kuangalia maendeleo ya mhusika, tathmini hali ya miwani na utimamu wake.
- Fanya marekebisho ya jumla na marekebisho mahsusi kama yatahitajika